

**TAARIFA YA MAENDELEO YA KAMPENI YA ONDOA MAPORI ONGEZA  
UZALISHAJI WILAYA YA MASASI KWA MH. GELASIUS BYAKANWA MKUU  
WA MKOA WA MTWARA TAREHE 23 DISEMBA 2020**

**1.0 Utangulizi**

Mhe. Mkuu wa Mkoa

Wilaya ya Masasi ina jumla ya hekta **280,696** zinazofaa kwa kilimo ambapo kati ya hizo Halmshauri ya Wilaya ina hekta **280,468.5** zinazolimwa kwa sasa ni hekta **184,935.5** sawa na asilimia 65.93. Halmashauri ya mji ina eneo linalofaa kwa kilimo lipatalo hekta **227.5** na zinazolimwa kwa sasa ni hekta 90 sawa na asilimia 40. Mazao ya kipaumbele ya biashara ni korosho, ufuta, alizeti, mbaazi, karanga na choroko. Aidha mazao ya chakula ni muhogo, mahindi, mpunga, mtama na mboga mboga.

**2. Uzalishaji wa korosho na ufuta**

Mhe Mkuu wa Mkoa,

Wilaya ya Masasi inakadiriwa kuwa na miti ya mikorosho ipatayo **4,868,365** ambapo Halmashauri ya Wilaya ina mikorosho **4,044,002** na Mji ina mikorosho ipatayo **824,363** (*Kiambatisho Na. 1 H/W na Kiambatisho Na. 2 H/M*).

Uzalishaji wa **korosho umeendelea kushuka** kwa takribani miaka mitatu kuanzia msimu wa 2017/2018 hadi 2020/2021. Hata hivyo uzalishaji wa **ufuta umeendelea** kuongezeka kuanzia msimu wa 2018/2019. Pamoja na ongezeko hilo la uzalishaji, Wilaya ya Masasi imejipanga kuongeza uzalishaji kwa kuendelea kutao hamasa

kupitia mikutano mbalimbali, vikundi na mkulima mmoja mmoja kwa kuanzisha mashamba mapya yenye kufuata kanuni bora za kilimo. Zifuatazo ni takwimu za uzalishaji wa korosho na ufuta kwa misimu mitatu iliyopita.

Masasi DC			Masasi TC	
Mwaka	Korosho (Kg)	Ufuta (Kg)	Korosho (Kg)	Ufuta (Kg)
2017/2018	28,757,957	2,065,804	9,065,556	123,023
2018/2019	26,618,589	4,854,912	5,984,236	288,546
2019/2020	26,191,454	6,151,388	6,444,220	365,502
2020/2021	25,214,162		5,263,365	-

### 3. Mkakati wa kuongeza uzalishaji na tija kwenye zao la korosho na ufuta.

**Mhe. Mkuu wa Mkoa,**

Katika kutekeleza kauli mbiu ya “ondoa mapori ongeza uzalishaji” Wilaya imetekeleza maazimio yaliyowekwa kama ifuatavyo: -

Na	Azimio	Utekelezaji
1	Kukufufua na kusafisha mashamba yaliyotelekezwa	<ul style="list-style-type: none"> <li>Kikao cha uzinduzi wa kampeni kifanyika tarehe 2/12/2020 ambapo WEOs, AMCOS na wadau wengine walialikwa.</li> <li>Watendaji wa kata na vijiji kwa kushirikiana na wenyeviti wa Vitongoji walianda orodha ya mashamba pori</li> </ul>
2	Kuundwa kwa kamati za hamasa kwa kila	Kamati za hamasa kwa ngazi ya Wilaya na kata zimeundwa. Kila kata ina kamati yake inayoongozwa na Mh. Diwani pamoja na Mtendaji wa kata. Kupitia

	Halmashauri, Tarafa na Kata.	mikutano ya vijiji wananchi wanaelekezwa kusafisha mashamba yao. Pia sheria ndogo za vijiji zitatumika kwa wasio safisha mashamba, na uchomaji wa moto mapori
3	Kutoa elimu ya matumizi sahihi ya viuatilifu pamoja na kutoa orodha ya viuatilifu vinavyofaa kutumika kwenye zao husika.	Maafisa ugani wanaendelea kutoa elimu rejea kwa wakulima kupitia mkulima mmoja mmoja au vikundi
4	Wilaya na Halmashauri zitengeneze mikakati na taratibu za kuwafanya vijana washiriki kwenye kilimo.	Uhamasishaji umefanyika katika vijiji vyote kuhusu vijana kushiriki katika shughuli za kilimo. Aidha, vijana wameshauriwa kutumia fursa ya uwepo wa mfuko wa mikopo katika Halmashauri kwa ajili ya kuanzisha miradi ya kilimo. Kila kijana ni lazima awe na shamba lisilopungua ekari moja
5	Vikundi vya uzalishaji miche vitambuliwe na kujengewa uwezo pamoja na wadau wengine kushiriki katika kuzalisha miche.	Vijana wamehamasishwa kuzalisha miche. Jumla ya miche 263 itazalishwa kwa msimu huu kupitia vikundi mbalimbali
6	Marufuku kwa wakulima kuandaa mashamba kwa kutumia moto.	Elimu inaendelea kutolewa kwa wananchi kupitia mikutano ya vijiji. Aidha, Mkuu wa Wilaya ameelekeza sheria ndogo za vijiji zitumike
7	Mamcu Ltd pamoja	Chama kikuu MAMCU na AMCOs zote za Wilaya ya Masasi walialikwa kwenye

	na AMCOS kushiriki kikamilifu kwenye mnyororo wa thamani kwenye mazao ya korosho na ufuta.	kikao cha hamsa na kupewa maelekeo kuwa kila kiongozi wa ushirika lazima awe na shamba.
--	--	---

Aidha, takwimu za mashamba ni kama ifuatavyo: -

Na	Mashamba	Masasi DC	Masasi TC
1	Maeneo yasiyolimwa	49,929 Ha	323.5 Ha
2	Mashamba yaliyotelekezwa	409 Ha	96 Ha
3	Mashamba mapya ya korosho	753 Ha	692 Ha
4	Mashamba mapya ya ufuta	3,232 Ha	150 Ha
5	Mahitaji ya Mbegu ya korosho	1,000 Kg	750Kg

## 5.0 HITIMISHO

Kwa mara nyingine tena naomba nichukue nafasi hii kukukaribisha tena katika Wilaya ya Masasi kwa ajili ya ziara yako ya kikazi na iwe yenye mafanikio katika kutimiza adhima na kauli mbiu ya **'ONDOA MAPORI ONGEZA UZALISHAJI**. Aidha nikukaribishe kwa maelekezo ambayo nakuahidi tutayafanyia kazi kwa haraka mara baada ya ziara yako.

Naomba kuwasilisha.